

Orodha Kaguzi ya Uthibitishaji

Tumia picha ambayo mwalimu wako anawasilisha kwa ajili ya zoezi hili ili kujibu maswali yaliyo hapa chini. Tafadhali tathmini kila kitu kwenye Orodha Kaguzi iliyo hapa chini kisha uandike majibu yako kwa kila swali. Fikiria nyenzo za mtandaoni au za nje ya mtandao unazoweza kutumia, nani unayeweza kuongea naye na vidokezi gani kwenye picha vinavyoweza kukusaidia kujibu kila swali.

1

ASILI:

Tafuta nakala ya asili ya picha hii na utambulisha wapi uliipata.

Kutambulisha asili ya picha hiyo kunaweza kuwa vigumu kwa wanafunzi kwa sababu bado hawajajifunza jinsi ya kufanya utafutaji picha kinyume. Ikiwa itakuwa vigumu kwa wanafunzi, waelekeze kwa kuwashauri wajaribu kutafuta nakala ya zamani zaidi ya picha hiyo.

Mwanahabari mweledi anaweza kuwasiliana na mpiga picha ili kuthibitisha iwapo picha hii ndiyo nakala ya asili.

2

CHANZO:

Tambulisha jina na jina la mtumiaji la mtu aliyepiga picha hii.

Majibu yanaweza kutofautiana.

3

TAREHE:

Tambulisha ni wakati gani picha hiyo ilipigwa. Tafadhali jumuisha mwezi, siku na mwaka.

Mwanahabari anaweza kuthibitisha hii zaidi kwa kuwasiliana na mhusika ili kuthibitisha.

4

MAHALI:

Tambulisha mahali ambapo picha hii ilipigiwa.

Wanafunzi wanaweza kuthibitisha hii kwa kuangalia vyanzo kadhaa vya habari.

5

NIA:

Orodhesha kile unachoamini kuwa ni chanzo na nia ya kupiga picha hii na kuisambaza.

Majibu yanaweza kutofautiana.

Chanzo: Maudhui haya yanahifadhiwa na Facebook na hivi sasa yanajumuisha mafunzo yaliyotolewa kwa shirika la Youth and Media katika Kituo cha Berkman Klein cha Intaneti na Jamii katika Chuo Kikuu cha Harvard chini ya leseni ya Kimataifa ya Creative Commons Attribution-ShareAlike 4.0. Unaweza kuyatumia maudhui hayo, ikiwa ni pamoja na kuyanakili na kuandaa kazi zinazotokana na maudhui hayo, kwa madhumuni ya kibiashara au la, ilimradi utataja mradi wa Youth and Media kama chanzo cha asili na kufuata masharti mengine ya leseni hiyo, kushirikisha kazi zingine zozote za ziada chini ya masharti hayo.